



# USAID

KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



Vikao vya awali vya vijana na Watoto vyenye lengo la kukusanya maoni kuhusu umri sahihi wa kupima VVU kwa hiari nchini Tanzania. Baada ya haya vijana walikutana na Kamati ya Bunge ya VVU na UKIMWI kutoa maoni yao

Picha kwa hisani ya: Mwanza Youth and Children's Network (MYCN)

## TANZANIA DATA-DRIVEN ADVOCACY

Mradi wa Data Driven Advocacy unalenga kuboresha na kudumisha uwezo wa asasi za kiraia (AZAKI) za Tanzania katika kushawishi mabadiliko chanya ya sera juu ya masuala ya haki za binadamu kwa kuhakikisha matumizi sahihi ya takwimu na taarifa. Data-Driven Advocacy itashiriki katika masuala anuwai ya kisekta, ikiwa ni pamoja na masuala ya haki za ardhi, ukatili wa kijinsia, haki ya elimu, makundi maalum ya watu katika jamii, wanawake na vijana.

Mradi huu una malengo makuu yafuatayo:

1. Kuimarisha ushirikiano na kushirikiana baina ya mashirika yenyeye nia na mtazamo mmoja juu ya kufanya utetezi kwa kutumia ushahidi.
2. Kuimarisha uwezo wa asasi za kiraia kukusanya, kutengeneza, kufuatilia, na kuripoti habari huru na za kuaminika juu ya masuala ya uvunjifu na ukiukwaji wa haki za binadamu.
3. Kuongeza uwezo wa AZAKI, mitandao na watu kushughulikia mahitaji ya dharura na yasiyotarajiwa.

Mradi wa Data Driven Advocacy unajenga uwezo wa mitandao na mashirika yanayolinda na kutetea haki za binadamu hasa yale yanayoongozwa na kutetea haki za wanawake, kushirikiana na serikali ya Tanzania katika kutekeleza masuala ya kipaumbele na kimkakati kwa kutumia mbinu za utetezi zilizojengwa katika ushahidi sahihi na wa kuaminika. Njia hii imejengwa katika dhana kuwa, wadau wa haki za binadamu wanaweza kuchangia utungwaji wa sera bora na jumuishi za masuala muhimu ya haki za binadamu kama wana; (1) utaalamu wa kutosha, taasisi imara na zenye uwezo, na wanapata ushauri endelevu (2) wanaweza kukusanya, kuchambua, kuwasilisha na kutumia takwimu katika kuanzisha kampeni za mabadiliko ya kisera kwa kutumia Ushahidi, (3) majukwaa wanayoweza kutumia katika kushirikiana na wadau mbalimbali pamoja na serikali.

Ingawa lengo kuu la Data-Driven Advocacy ni kufanya kazi kitaifa, mradi pia umeainisha masuala ya haki za binadamu yanayotakiwa kufanyiwa kazi katika ngazi ya mkoa. Mikoa ya kipaumbele kwa sasa ni Dodoma, Arusha, na Zanzibar.

## MATOKEO

- Serikali ya Tanzania inaonesha ukubali wa kazi za utetezi zinazofanywa na AZAKI juu ya masuala muhimu ya haki za binadamu kutokana na uwepo wa ushahidi thabiti unaowasilishwa kwa sauti na asasi za kiraia.
- Angalau mitando minne ya AZAKI imetengeneza na inafanya kazi mikakati ya utetezi wa masuala ya kipaumbele ya haki za binadamu na inashughulikia masuala haya kwa kushirikiana na wanahabari, sekta binafsi, na washirika wa kiserikali.
- Angalau uwezo wa kitaasisi wa AZAKI 53 zinazoshughulikia masuala ya haki za binadamu unaimarishwa kuititia ushauri endelevu, ambao ni muhimu katika kuhakikisha ufanisi na udumishaji wa mipango ya utetezi.
- Angalau AZAKI 10 zimejengewa uwezo wa kubaini changamoto na fursa zinazohusiana na masuala ya haki za binadamu na zimetengeneza mikakati ya kukabiliana na masuala yenyе ucharaka yatayojitekeza.

**BAJETI** Dola za Marekani milioni 8.7

### MUDA

Agosti 2017 – Agosti 2022

### MAENEKO YA MRADI

Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, and Zanzibar; mikoa ya ziada inaweza kuongezwa

### MTEKELEZAJI

Freedom House  
PACT

### WASHIRIKA WAKUU

- National Council of NGOs (NACONGO)
- Tanzania Human Rights Defenders' Coalition
- Women In Law and Development Africa
- Union of Tanzania Press Clubs/Arusha Press Clubs
- Association of Non- Governmental Organizations in Zanzibar
- The Tanganyika Law Society (TLS)
- Mwanza Youth and Children's Network (MYCN)
- PINGOs Forum
- Zanzibar Legal Services Center (ZLSC)
- Ujamaa Community Resource Team (UCRT)
- Pastoral Women's Council (PWC)
- Vijana Pambana Pata Maendeleo Rukwa (VIPAMARU)
- Pemba Association of Civil Society Organizations (PACSO)

### MAWASILIANO YA USAID

Adam Lingson  
Afisa Mwakilishi wa Mkataba  
+255 22 229 4806  
[alingson@usaid.gov](mailto:alingson@usaid.gov)

### MAWASILIANO YA MTEKELEZAJI

Daniel Naftal Lema  
Mkuu wa Mradi  
[Lema@freedomhouse.org](mailto:Lema@freedomhouse.org)

### KWA MAWASILIANO ZAIDI

Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)  
Facebook: USAIDTanzania  
Twitter: @USAIDTanzania